# Ujitokezaji wa Viambishi vya Nafsi katika Kiarabu, Kitumbatu na Kiswahili

*Sauda Uba Juma*
*Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere*

**Ikisiri**

**Makala haya yanalenga kuchunguza ujitokezaji wa viambishi vya nafsi katika Kiarabu Kitumbatu na kuvilinganisha na Kiswahili. Lengo la uchunguzi huo ni kutaka kubaini jinsi vipengele hivyo vinavyoingiliana na kusigana. Hii inatokana na ukweli kwamba mapisi ya lugha ya Kiswahili na lahaja zake pamoja na lugha ya Kiarabu mpaka sasa hayajatindimaa kwa kuwa lugha hizi zilikuwa na mtagusano na muasala wa muda mrefu tangu 800 BK. Kutokana na hali hiyo kumeibuka mitazamo kinzani juu ya uhusiano wa Kiswahili na Kiarabu. Kuwepo kwa baadhi ya maneno ya Kiarabu katika Kiswahili kumechochea hoja kwamba Kiswahili kinatokana na Kiarabu. Mjadala huo ni wa muda mrefu ambao unaendelea hadi sasa. Baadhi ya tafiti tangulizi zimebainisha idadi kubwa ya maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu. Hata hivyo, mfanano huo wa kimsamiati baina ya Kiswahili na Kiarabu haujitoshelezi kutoa hitimisho juu ya chimbuko la Kiswahili. Baadhi ya watafiti waliochunguza maneno ya Kiarabu katika Kiswahili wamebaini kuwapo kwa asilimia kubwa ya mfanano wa kategoria ya nomino baina ya lugha hizi mbili kuliko katika kategoria zingine. Hivyo pamoja na kuwepo kwa kategoria mbalimbali za maneno, utafiti huu umejibana kushughulikia jinsi viambishi vya nafsi vinavyojitokeza katika kategoria ya vitenzi vya Kiarabu, Kitumbatu na kuvilinganisha na Kiswahili. Hii ni kwa sababu kwa kuwa imeshatibitika kwamba, Kitumbatu ni miongoni mwa lahaja ya Kiswhili, ujitokezaji huo wa viambishi utatupa mwanga kati ya uhusiano wa Kiarabu na Kiswahili. Chanzo ya data za utafiti huu zimekusanywa kupitia usomaji wa nyaraka, vitabu na kamusi mbalimbali zilizoandikwa kuhusu kategoria hiyo. Vilevile, tulipitia nyaraka hizo ili kupata maarifa ya jumla kuhusu ujitokezaji wa viambishi vya nafsi kwa mujibu wa waandishi mbalimbali. Data zingine zilikusanywa uwandani kupitia mbinu ya usaili na hojaji kwa wazungumzaji wa Kiarabu na Kitumbatu. Aidha utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Fonolojia Umbo Upeo kuanzia sasa (UU). Kwa ujumla matokeo ya utafiti huu yameonesha kwamba Kitumbatu kina uhusiano zaidi na Kiswahili kuliko Kiarabu. Hii ni kudhihirisha kwamba Kiswahili na Kiarabu ni lugha mbili ambazo hazina uhusiano wa kimnasaba kwa kuwa hazikuchipukia kutoka kwenye lugha yenye asili moja.**

**Maneno Muhimu:** *Viambishi, Kategoria, Mapisi, Kusigana, Hayajatindimaa, Muasala*

## Utangulizi kuhusu Viambishi

Viambishi nafsi ni kipengele katika lugha ambacho kimeshajadiliwa na waandishi mbalimbali katika lugha ya Kiswahilli. Miongoni mwao ni: Mgullu (1999), Kihore na wenzake (2003), Chomi (2017), Habwe na Karanja (2012) na Matinde (2012). Waandishi hawa wameelezea kuhusu viambishi kwa ujumla, ambapo pia wamezungumzia viambishi vya nafsi katika Kiswahili. Katika makala haya tunajadili jinsi viambishi vya nafsi vinavyojitokeza katika Kiarabu, Kitumbatu na kuvilinganisha na Kiswahili. Kitumbatu ni lahaja inayozungumzwa katika kisiwa cha Tumbatu kilichoko kaskazini mahariki mwa kisiwa cha Unguja. Kisiwa hiki kiko umbali wa kilomita 40 kutoka mjini Unguja. Wakazi wa asili wa kisiwa hiki wanajulikana kama Watumbatu ambao inaaminika kwamba, lahaja yao haijaathirika na lugha zingine za kigeni pamoja na Kiswahili sanifu Juma (2019). Makala haya yamegawanyika katika sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza inahusu taarifa tangulizi kuhusu dhana ya viambishi, aina za viambishi na vitenzi ili kuweka msingi madhubuti wa kuielewa makala haya. Sehemu ya pili, inahusu mwenga wa kinadharia uliotumika kuongoza uchambuzi wa data. Sehemu ya tatu inahusu methodolojia iliyotumika katika ukusanyaji wa data. Sehemu ya nne inajadili matokeo ya utafiti kwa ujumla na sehemu ya tano ambayo ni ya mwisho inahusu hitimisho la makala. Sehemu inayofuata inafafanua dhana za msingi katika makala haya.

**Dhana ya Viambishi**

Maana ya viambishi imeshafasiliwa na wanazuoni mbalimbali kulingana na mitazamo yao. Baadhi ya waandishi wanataja mofimu badala ya viambishi, hii inatokana na ukweli kwamba mofimu pia huweza kuwa viambishi wakati mwingine hasa zile mofimu tegemezi. Hivyo dhana ya viambishi na mofimu zinakaribiana sana kiumbo ingawa zinatofautiana kiuamilifu wake. Kwa mtazamo huo viambishi vyote ni mofimu lakini si kila mofimu ni viambishi hususani mofimu huru. Hebu sasa tutalii fasili chache za wanazuni mbalimbali kuhusu maana ya viambishi.

Kwa mujibu wa Mgullu (1999) kiambishi ni istilahi ambayo hutumiwa hasa katika uwanja wa mofolojia kuelezea sehemu mbalimbali za maneno ambazo huongezwa (huambishwa) katika mizizi ya maneno. Istilahi yenyewe ni angavu kwa sababu katika lugha ya Kiswahili kuambisha ni kuongeza au kuweka kitu fulani juu ya kitu kingine. Hivyo viambishi ni mofu ambazo huongezwa kwenye mizizi ya maneno na viambishi hivyo huwakilisha maana fulani. Katika lugha nyingi viambishi huwa na maana ya kisarufi zaidi na havina maana za kileksika.

Kwa upande wao Kihore na wenzake (2003) kiambishi ni mofimu zinazoambatanishwa kwenye mzizizi wa neno ili kuwakilisha hali au dhana mbalimbali zinazofungamana na neno pamoja na mofimu hizo. Katika lugha ya Kiswahili viambishi huweza kujitokeza tu mwanzoni au mwishoni mwa mzizi. Aidha, wanaendelea kudai kwamba katika lugha nyingine za Kibantu viambishi, mbali na kuweza kujitokeza mwanzoni mwa mzizi funge, huweza kujitokeza ndani ya mzizi funge wenyewe. Hii ina maana kwamba baadhi ya lugha za Kibantu upachikwaji wake wa viambishi uko tofauti na wa lugha ya Kiswahili. Katika utafiti huu tumechunguza kama utaratibu huo wa ujitokezaji wa viambishi unafanana au unatofautiana katika Kitumbatu na Kiarabu.

Katika makala haya kiambishi kinafasiliwa kama ni vijineno vinavyoambikwa kabla na baada ya mzizi wa neno ili kuleta uarifishaji mkamilifu. Viambishi vinaweza kugawanywa katika makundi mbalimbali si lengo la utafiti huu kuchunguza makundi yote hayo ya viambishi. Utafiti huu ni mahususi ambapo umejikita kuchunguza viambishi vya nafsi vinavyojitokeza katika Kiarabu, Kitumbatu na kuvilinganisha na Kiswahili. Utafiti wa maktabani umedhihirisha kwamba viambishi nafsi katika Kiswahili vimeshachunguzwa na baadhi ya wanazuoni. Data katika tafiti hizo zimetusaidia kuzilinganisha na Kitumbatu pamoja na Kiarabu ili kubaini namna zinavyoshikana na kuachana. Hii ni kwa sababu hakuna data za kutosha zinazoonesha jinsi viambishi vya nafsi vinavyojitokeza katika Kitumbatu na Kiarabu.

**Uainishaji wa Viambishi**

Viambishi huweza kuainishwa kwa namna mbili tofauti. Namna ya kwanza ni kuvianisha kwa kufuata maumbo yake na nafasi vinamotokea. Namna ya pili ni kuvianisha kwa kuzingatia uamilifu wake kama vipengele vya kisarufi. Uainishaji wa viambishi kiumbo, huwa tunaangalia jinsi viambishi hivyo vilivyojengeka na vinachukua nafasi gani katika neno. Uanishaji wa kiuamilifu au kikazi, huwa tunaangazia kazi zinazofanywa na viambishi mbalimbali kutegemea na mahali kilipo katika umbo la neno na vilevile aina ya neno kilimojitokeza. Baadhi ya kazi za viambishi ni uwakilishi wa njeo, nafsi, ukanushi, hali n.k. Viambishi vyote hivyo vinaweza kuingizwa katika makundi mawili makuu ambayo ni viambishi awali na viambishi tamati.

Akizungumzia kuhusu viambishi awali Matinde (2012) ana haya ya kusema: Viambishi awali hutokea mwanzoni mwa kitenzi kabla ya mzizi wa neno. Viambishi hivyo huwa katika aina mbalimbali kama vile viambishi awali vya njeo, nafsi, ukanushi, mtenda, ngeli n.k. Hivyo, katika utafiti huu tumejikita na kuchunguza ujitokezaji wa viambishi vya nafsi tu. Aina nyingine za viambishi zimetajwa tu bila kufafanuliwa kwa kina pale ilipotulazimu kufanya hivyo. Viambishi vya nafsi kwa kawaida huonesha nafsi ya msemaji na pia iwapo nafsi inayozungumziwa ni umoja au wingi. Vilevile, vinaweza kuwa katika hali ya uarifu au ukanushi. Hivyo, uamilifu wa viambishi unaweza kujitokeza katika nomino au vitenzi hata hivyo, viambishi vya nafsi huwa na tabia ya kuandamana na vitenzi ambavyo vinaweza kujitokeza mwanzoni kabla ya mzizi wa kitenzi. Kwa msingi huo, kitenzi ni kategoria ya msingi katika ujitokezaji wa viambishi mbalimbali. Kipengele kinachofuata tumefafanua kuhusu vitenzi.

**Dhana ya Vitenzi**

Maana ya kitenzi imefasiliwa na wataalamu kadha wa kadhaa kama ifuatavyo: BAKIZA (2010) wanaeleza kwamba kitenzi ni kipashio katika sentensi kinachoeleza tendo linalofanyika. Naye Nyangwine (2002) anafafanua kwamba kitenzi kinaeleza jambo linalotendwa au linalotendeka. Kitenzi huarifu tendo linalofanyika au linalofanywa na mnyama, mtu au kiumbe chochote kinachoweza kutenda jambo kama vile *soma, andika simama, cheza, kunywa* n.k. Vitenzi vya Kiswahili havisimami pekee vinapotumiwa katika tungo bali huambatana na viwakilishi vingine vyenye kuwakilisha mtenda wa tendo linapofanyika kwa mfano 1:

| **Nomino/Kiwakilishi** | **Kitenzi** |
|---|---|
| i. Mimi | ni-li-som-a |
| ii. Mwalimu | a-na-andik-a |
| iii. Kaka | a-ta-lim-a |
| iv. Wanafunzi | wa-na-chez-a |

Katika mfano huo tunabaini kwamba kitenzi katika Kiswahili kinaambikwa viambishi mbalimbali vyenye dhima mahususi katika tungo. Viambishi hivyo huweza kuwakilisha mtenda, nafsi, ukanushi, ngeli, idadi, hali n.k.

Khamis na Kiango (2002) wanaeleza kuwa kitenzi ni istilahi inayowakilisha neno kuu linaloelezea tendo linalotendwa na kiima cha sentensi. Kazi hiyo inaweza kuwa kuwaza, kutenda na kuwasiliana kwa sauti. Kwa mfano *Juma* ***anafikiri*****,** *Juma* ***anachuma*** *kahawa* na *Juma* ***anasema.*** Wanaendelea kudai kuwa kitenzi kinaweza kuhusisha kiima na aina nyingine za maneno kama kiima au kivumishi. Kwa mfano *Asha* ***ni*** *mhandisi, ni* kitenzi kinachohusisha nomino *Asha* na nomino *mhandisi.* Katika mifano hiyo maneno *anafikiri, anachuma* na *anasema* vinawakilisha seti ya vitenzi vyenye kuonesha tabia fulanifulani za kisemantiki, kisintaksia na za kimofolojia. Vitenzi vina tabia mbalimbali kwa mtazamo wa Khamis na Kiango, kitenzi kinachojipambanua kimofolojia ni kile ambacho kinahusisha kiima cha sentensi na nomino au kivumishi ambacho ni *ni* mathalani *Ali* ***ni*** *daktari* na *Asha* ***ni*** *tajiri.*

Uhusishaji huu wa kitenzi *ni* baina ya kiima, nomino au kivumishi unajikita zaidi katika wakati uliopo. Endapo uhusishaji huu utakuwa wa mambo yaliyotokea zamani, umbo la *ni* hutoweka na umbo la *wa* linachukua nafasi yake. Kwa mfano *Ali* ***alikuwa*** *daktari na Asha* ***alikuwa*** *tajiri.* Vilevile, kama uhusishaji huo utakuwa ni ule wa atiati yaani usiokuwa na uhakika umbo la kitenzi pia hubadilika. Tungo kama hizo zinaweza kuwa *Ali* ***angekuwa*** *daktari* au *Asha* ***angekuwa*** *tajiri.* Hivyo, ni dhahiri kwamba kitenzi husishi kinaweza kuwa na sura zaidi ya moja ambazo zinategemea mazingira ya kisarufi ya utokeaji wake.

Vitenzi vingine huonesha mabadiliko ya kimofolojia lakini haviathiriwi sana katika umbo kama kilivyo kitenzi husishi. Mara nyingi mabadiliko haya hayagusi mzizi wa kitenzi bali huongeza viambishi kabla na baada ya mzizi wa kitenzi. Kwa kawaida kitenzi cha Kiswahili kinakuwa na mzizi na kiambishi tamati ambacho siku zote huwa ni cha irabu. Mfano 2:

| **Kitenzi** | **Mzizi** | **Kiambishi Tamati** |
|---|---|---|
| *soma* | *som* | *a* |
| *lima* | *lim* | *a* |
| *lala* | *lal* | *a* |
| *cheza* | *chez* | *a* |

Kiujumla maumbo ya kitenzi yanaweza kubadilikabadilika katika upachikwaji wake wa viambishi kutegemaea na hali ya kimazingira tofautitofauti.

Chomi (2017) anasema kuwa kitenzi kinaarifu, yaani kinatoa taarifa juu ya mtenda wa tendo, juu ya mtendwa wa tendo katika sentensi. Kwa mantiki hii kitenzi hujulikana kama kiarifu kama kinavyojitokeza katika mifano ifuatayo: *Mussa* ***anapika*** *chakula, matunda* ***yalichumwa****, mama* ***anawapikia*** *watoto uji* n.k. Vitenzi *anapika, yalichumwa na anawapikia* ni mifano ya vitenzi. Kwa mujibu wa Chomi kitenzi hutoa taarifa juu ya wahusika wote katika sentensi na sio taarifa juu ya kiima tu kama inavyoelezwa katika sarufi za kimapiokeo.

Chomi (2013) anafafanua kwamba kimofolojia kitenzi katika Kiswahili ni muundo wa mzizi tenzi pamoja na kiambishi tamati kimoja au zaidi ambacho hujuilikana kama kitenzi cha msingi (taz. § mfano 1). Kitenzi pia kinaweza kuwa cha mnyumbuliko ambacho huwa na muundo wa mzizi tenzi pamoja na viambishi tamati angalau viwili, kimoja kikiwa kiishilizi. Katika kitenzi cha msingi au cha myumbuliko huweza kuongezwa kiambishi awali kimoja au zaidi na kuunda tungo kama ifuatavyo:
Mfano 3:

| Kitenzi cha Msingi | Kitenzi cha Mnyumbuliko |
|---|---|
| *anasoma* | *ananisomesha* |
| *wataimba* | *wataimbisha* |
| *tumecheza* | *tutamchezesha* |
| *hakusoma* | *hakumsomea* |
| *hawataimba* | *waliimbisha* |

Hivyo tungo katika mfano 3 si vitenzi tu bali ni tungo tenzi ambazo pia zina sifa za kisentensi. Kwanza tungo hizo zimebeba viambishi patanishi kama vile *a-, wa-, tu-, ni-, ha-* n.k. Viambishi hivyo vinasababisha tungo tenzi kuwa na hadhi ya kisentensi. Katika makala haya tumejikita na kuangazia zaidi jinsi ujitokezaji wa viambishi vya nafsi unavyolandana na kusigana baina ya Kitumbatu, Kiarabu na Kiswahili.

**Mwega wa Kinadharia**

Utafiti huu, umeongozwa na nadharia ya Fonolojia Umbo Upeo (UU). Kiunzi hiki cha kinadharia kilianzishwa na Prince na Smolensky (1993) na kuendelezwa na Prince na McCarthy (1993). Lengo lake kuu ni kuzitalii kanuni za kimajumui za lugha, namna ya kuziainisha na jinsi ya upataji lugha. Vilevile nadharia hii ilianzishwa ili kupunguza udhahania uliokithiri wa uwakilishi wa vipengele vya kifonolojia katika kulikokotoa umbo la ndani kutoka umbo la nje kwa kutumia sheria na kanuni. Katika muktadha huo, UU awali ilianzishwa ili kutatua matatizo ya kifonolojia lakini baadaye ikapanuliwa kwa kushughulikia masuala ya vipengele vingine vya kiisimu kama vile mofolojia na sintaksia (Massamba, 2011).

Madai muhimu ya UU ni kwamba miundo mbalimbali ya lugha hutokana na ukinzani baina ya mashartizuizi; kwa maana ya kutofautiana kwa thamani ya mashartizuizi katika mpangilio ama wa sauti, maneno au virai. Mashartizuizi (MASHA-ZU) ni masharti yatuelekezayo kwamba tukitaka kupata umbo fulani sharti tufanye au tusifanye jambo fulani. Kwa hakika, kuna MASHA-ZU ya aina mbili. Mosi, MASHA-ZU ya uadilifu ambayo huhitajia kwamba umbotokeo kwanza likubalike na pia lifanane na umboghafi lililoingizwa. Hii ina maana kwamba mashartizuizi haya yahitajia pawepo na mshabaha baina ya maumboghafi na maumbotokeo. Pili, MASHA-ZU ya uziada ambayo yanakubali mabadiliko na kuruhusu ukiukwaji wa baadhi ya MASHA-ZU yanayovumilika, hivyo kulifanya umbo likubalike.

Nadharia ya UU inafanya kazi kwa kuzingatia misingi mikuu minne (4). Nayo ni Umajumui, Ukiukwaji, Upangiliaji na Usambamba. Sarufi Majumui ina seti ya MASHA-ZU ambayo ni ya kimajumui na yanayopatikana katika sarufi za lugha zote. Ukiukwaji wa MASHA-ZU unawezekana, lakini ukiukwaji huo huwa ni wa kiwango kidogo; kwani ukiukwaji ukizidi utatupa lugha nyingine tofauti kabisa. Upangiliaji MASHA-ZU huweza kuwa katika mpangilio wa unguvu na uhafifu wake kwa kuzingatia misingi ya lugha mahsusi. Maumbotokeo ambayo yanakiuka MASHA-ZU hafifu, huwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kufikia upeo wa ukubalifu kuliko yale yaliyokiuka MASHA-ZU yenye nguvu. Katika Usambamba, unaweza kuwa na utoshelevu wa mpangilio wa MASHA-ZU ambao huangaliwa kwa kutazama seti nzima ya maumbotokeo yanavyojidhihirisha katika mpangilio wote nzima.

Tathmini (TATH) ndiyo sehemu inayoamua umbotokeo lipi limeshinda; yaani limefikia upeo wa ukubalifu (linakubalika zaidi). Hii ina maana kwamba, umbo likifikia upeo wa ukubalifu huwa halikiuki masharti yoyote au linakiuka mashartizuizi hafifu zaidi kati ya idadi ya maumboshindani yaliyotathminiwa kutegemea na mpangilio wa MASHA-ZU katika lugha mahusuis. ZALI huzalisha

maumbo kutokana na maumboghafi; hatimaye huzalisha idadi isoukomo ya maumbotokeo au maumboshindani.

Baadhi ya seti ya MASHA-ZU katika Kiswahili ni kama ifuatayo:

| | |
|---|---|
| *KKK | Mfuatano wa konsonanti tatu halisi katika maneno yasiyo ya mkopo haukubaliki |
| *KYK | Mfuatano wa konsonanti, kiyeyusho na konsonanti haukubaliki |
| *H-KODA | Silabi haiwezi kuwa na koda (silabi kuishia na konsonanti) |

Hebu tuchunguze mfano ufuatao:

Katika mchakato huu umbotokeo baiskeli ndilo umbo lililoshinda na kufikia upeo wa ukubalifu, kwani ndilo umbo pekee ambalo halikuvunja MASHA-ZU yenye nguvu kulingana na mpangilio wa lugha ya Kiswahili.

Mchakato huu unajitokeza katika Jedwali Na. 1 kama ifuatavyo:-

MASHA-ZU: K(Y)KK >> FIKI-UKO >> TEGE >> SHABI

| Ingizo | Maumbo Shindani | K(Y)KK | FIKIUKO | H-KODA | TEGE |
|---|---|---|---|---|---|
| Baiskeli | a) bicycle | **! | * | | * |
| | b) ☛baiskeli | | | | |
| | c) bayskeli | *! | | * | * |
| | d) baiskel | | * | * | |

Umbo (b) ndilo lililoshinda kwa kuwa halijakiuka masharti yoyote. Umbo (a) limekiuka sharti lenye nguvu kuliko maumbo yote, kwa kuwa utaratibu huo haukubaliki katika lugha ya Kiswahili na lahaja zake, likifuatiwa na umbo (c). Umbo (d) lina uwezo mkubwa zaidi wa kuchaguliwa kuliko umbo (a) na (c). Lakini umbo hili halikuchaguliwa kwa sababu kuna umbo (b) ambalo halikukiuka sharti lolote Sharti lenye nguvu huja mwanzo na hafifu zaidi huja mwisho.

UU ina nadhriatete ya Utangamano, ambayo inaweka seti ya MASHA-ZU ambayo hufanya pawepo na mshabaha baina ya umboghafi na umbotokeo. Kadhalika, huzuia udhahania wa hali ya juu na kulinda uadilifu. Nadhariatete hii inahusu vitu vitatu; Fikia ukomo wa ukubalifu (FIKI-UKO) ambayo ni familia ya masharti ya utangamano. Masharti haya huweka ukomo kwenye kiwango cha udhahania baina ya umboghafi na umbotokeo, kwa kuhitajia kwamba kila kipandesauti cha umboghafi pia kijitokeze katika umbotokeo. Masharti haya, huzuia udondoshaji wa kipandesauti chochote kilichokuwa katika umboghafi. (TEGE): Tegemea ni familia ambayo, inaweka ukomo wa kiwango cha udhahania baina ya umboghafi na umbotokeo. Huhitajia kwamba kila kipandesauti cha umbotokeo pia kijitokeze katika umboghafi, hivyo huzuia uchopekaji. (SHABI): Mshabaha ni masharti ya utangamano ambayo yahitajia kwamba kila kipandesauti kilichomo katika umbotokeo kifanane na kipandesauti chenzie katika sifa zinazokiuda.

Nadharia hii imejaribu kuonyesha seti ya MASHA-ZU inayoweza kujitokeza katika viambishi vya nafsi vya Kiarabu, Kitumbatu na Kiswahili. Kwa mshabaha huo tumeweza kugundua mashartizuizi gani yanavumilika na yapi hayavumiliki kulingana na jinsi viambishi vya vya nafsi vinavyojitokeza katika hizo, kulingana na wazungumzaji.

**Methodolojia**

Data za makala haya zimepatikana kutoka katika vyanzo mbalimbali kuhusu ujitokezaji wa viambishi vya nafsi katika lugha ya Kirabu, Kitumbatu na Kiswahili. Hii ni kwa sababu utumiaji wa mbinu zaidi ya moja huifanya data iweze kuaminika zaidi Dawson (2007). Utafiti huu ulikusanya data kutoka kwa watu mbalimbali ambao ni sehemu ya jamii ya watumiaji wa lugha ya Kiarabu, Kitumbatu na Kiswahili,. Njia mahususi tatu zilitumika katika ukusanyaji wa data za makala haya. Kwanza, tulitumia mbinu ya udurusu wa nyaraka mbalimbali zilizohusu viambishi vya nafsi ambapo kamusi mbalimbali za Kiswahili na Kiarabu zilitumika. Mbinu ya pili ilikuwa ni usaili ambapo mtafiti

alifanya mahojiano na watu mbalimbali ambao ni wamahiri wa lugha ya Kiswahili, lugha ya Kiarabu na Kitumbatu ili kubaini jinsi viambishi vya nafsi vinavyojitokeza katika tungo mbalimbali wakati wa mahojiano hayo. Watu hao walichaguliwa kwa kutumia njia ya usampulishaji lengwa kupitia umahiri wao wa lugha. Jambo hili lilifanikiwa kupitia watafiti wasaidizi pamoja na utafiti wa awali tulioufanya. Mbinu ya tatu iliyotumika katika makala haya ni hojaji. Hojaji hizo zimehusisha miundo mbalimbali ya tungo zenye viambishi vya nafsi zilizoandikwa kwa Kiswahili ambapo watoataarifa walitakiwa kuzijaza kwa kulingana na utaratibu wa lugha zao.

Watoataarifa 10 waliojaza hojaji ni wajuzi wa lugha wanaojua kusoma na kuandika Kiswahili na Kiarabu kutoka katika Chuo cha Kiislamu kilichopo Kiembe Samaki wilaya ya Magharini B Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja. Hojaji pia zilijazwa na wazungumzaji wa Kitumbatu katika kisiwa cha Tumbatu. Hojaji ni mbinu rahisi ya kukusanya taarifa kutoka kwa watoataarifa wengi kwa wakati mmoja Ponera, (2019). Hivyo basi, inaokoa muda kwa kupata taarifa nyingi kwa muda mchache na hutunza siri za watafitiwa. Kwa kutumia mbinu ya hojaji, data ilikusanywa na majumuisho yalifanywa kutokana na matokeo ya data husika.

Mtafiti pia, alikusanya data kupitia mbinu ya usaili ambayo ni mbinu ya ukusanyaji wa taarifa inayohusisha uulizaji wa maswali kwa njia ya mdomo, majadiliano, majibizano ya ana kwa ana au kwa njia ya simu. Lengo likiwa kukusanya taarifa na maoni kutoka kwa watafitiwa kuhusiana na suala la kiutafiti. Shabaha ya kutumia mbinu hii ni kulinganisha na kuchunguza mlingano na mtazamo wa watafitiwa kuhusu viambishi vya nafsi katika lugha ya Kiswahili, Kitumbatu na Kiarabu. Sehemu inayofuata inafafanua kuhusu dhana ya viambishi vya nafsi.

**Viambishi Nafsi**

Nafsi ni kipashio cha lugha kinachodhihirisha mhusika katika usemaji TUKI (1990). Viambishi nafsi ni mofimu ambazo huungwa kwa viambishi awali katika vitenzi na huashiria mtendaji wa kitendo kinachohusika Habwe na Karanja (2012). Kiarabu na Kitumbatu kama zilivyo lugha nyingine duniani zina kategoria mbalimbali za maneno kama vile nomino, vitenzi, vivumishi, viwakilishi, vielezi n.k. Si lengo la utafiti huu kuchunguza aina zote hizo za maneno katika Kiarabu na Kitumbatu. Makala haya yamejikita katika kuchunguza ujitokezaji wa viambishi vya nafsi tu katika Kiarabu na Kitumbatu kisha kuvilinganisha na Kiswahili. Lugha ya Kiarabu ina aina kuu 3 za nafsi ambazo ndani yake zinapatikana nafsi 12 katika umoja na wingi. Katika lugha hiyo nafsi hizo zinajulikana kama *dhamir* (نمر). Vilevile, katika Kiarabu nafsi hizo zinatofautisha jinsi kama ni mwanamke au mwanamme. Ufafanuzi wa nafsi hizo ni kama ifuatavyo katika Jedwali Na. 2:

| Nafsi | Kiarabu | | Kitumbatu | | Fasiri katika Kiswahili | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Umoja | Wingi | Umoja | Wingi | Umoja | Wingi |
| 1 | *anaa (أ)* | *nahnu (نحن)* | *miye* | *suye* | mimi | sisi |
| 2 | *anta (انت)* | *antum (انم)* | *weye* | *nyuye* | wewe (me) | nyinyi |
| | *anti (أنت)* | *antunna (أتئا)* | | | wewe (ke) | nyinyi |
| 3 | *huwa (هو)* | *hum (هم)* | *weye* | *nyuye* | yeye (me) | wao |
| | *hiya (هي)* | *hunna (هئا)* | *veye* | *veo* | yeye (ke) | wao |
| 2 | - | *antumma (هما)* | - | - | - | - |
| 3 | - | *humma (هفا)* | - | - | - | - |

Katika Jedwali Na. 2 tunabaini nafsi 12 ambazo zinatumika katika lugha ya Kiarabu katika umoja na wingi. Hii ni tofauti na Kitumbatu pamoja na Kiswahili ambazo zina aina 3 kuu zenye nafsi 6 tu pia, hazitofautishi jinsi ya kike wala ya kiume kama ilivyo katika Kiarabu. Hivyo, kama ambavyo tumetangulia kusema kwamba makala haya yanalenga kuchunguza ujitokezaji wa viambishi nafsi katika lugha ya Kiarabu, Kitumbatu na kuvilinganisha na Kiswahili. Ulinganishi ambao umetupa fununu ya uhusiano wa lugha hizo kimnasaba. Katika makala haya viambishi hivyo vitaangaziwa katika wakati uliopo, wakati uliopita na wakati ujao. Tutatumia vitenzi 2 au 3 kwa kila wakati uliobainishwa kutokana na ufinyu wa nafasi katika jarida.

**Kiambishi Nafsi cha Wakati Uliopo**

Masebo na Nyangwine (2002) wanafafanua kwamba katika lugha ya Kiswahili, njeo ya wakati uliopo huwakilishwa na kiambishi *-na-* na *-i-* ambapo kinaonesha kwamba tendo linaendelea kutendwa sasa. Kiambishi *-na-* kinatumiwa kabla ya mzizi wa vitenzi yakinishi wakati kiambishi *-i-* kinatumiwa katika vitenzi vinavyokanusha na huambishwa mwishoni mwa kitenzi kama kiambishi tamati. Data ifuatayo inaonesha jinsi kiambishi cha nafsi kinavyojitokeza katika vitenzi vya Kiarabu na Kitumbatu katika wakati uliopo. Tuchunguze mfano wa 4 unaoonesha jinsi viambishi vya nafsi vinavyojitokeza katika wakati uliopo:

| ***Kiarabu*** | ***Kitumbatu*** | ***Fasiri ya Kiswahili*** |
|---|---|---|
| *adhhabu (اذهب)* | *nda* | *ninakwenda* |
| *nadhhabu (نذهب)* | *tunda* | *tunakwenda* |
| *tadhhabu (تذهب) (ke)* | *kanda* | *anakwenda* |
| *naktubani (يَكْتُبُوْنَ)* | *mwandika* | *mnaandika* |

Katika wakati uliopo tumechunguza ujitokezaji wa viambishi vya nafsi katika vitenzi *ninakwenda*, *tunakwenda* na *anakwenda*. Tukianza na (*ninakwenda),* kitenzi hiki kimepachikwa kiambishi cha nafsi -*ni*- ambacho kinaonesha nafsi ya 1 umoja na kiambishi *na*- kinachoonesha wakati uliopo katika Kiswahili. Kadhalika katika Kitumbatu kitenzi *ninakwenda* (*nda)* kiambishi *n*- kinaonesha nafsi ya kwanza umoja wakati huohuo kinaonesha wakati uliopo. Katika Kiarabu *ninakwenda adhhabu (اذهب)* kiambishi -أ *(a)* cha nafsi ya 1 umoja kimewakilisha pia njeo ya wakati uliopo. Hii inadhihirisha kwamba kila lugha ina upekee wake katika kuyapanga maneno kwa mujibu wa utaratibu wa lugha husika. Kwa mnsaba huo, ujitokezaji wa viambishi pia unaweza kulingana au kutofautiana. Hivyo, endapo utaratibu huo utakiukwa ndipo tunaposema kuna ukiukwaji wa MSHA-ZU katika lugha hiyo. Katika Kiarabu na Kitumbatu masharti hayo yanafafanuliwa kama ifuatavyo:

*Knf1uKwo >> FIKI-UKO >> TEGE>> SHABI

| | |
|---|---|
| *Knf1uKwo | Kiambishi nafsi ya kwanza umoja hakiwezi kufuatiwa na kiambishi cha wakati uliopo |
| FIKI-UKO | kila kipandesauti cha umboghafi kijitokeze katika umbotokeo (hakuna udondoshaji) |
| TEGE | kila kipandesauti cha umbotokeo pia kijitokeze katika umboghafi (hakuna uchopekaji) |
| SHABI | kila kipandesauti cha umbotokeo kishabihiane na chenzie katika sifa zinazokiunda. |

Tuchunguze namna maumbo shindani yanavyokiuka MASHA-ZU kutoka katika Jedwali Na. 3 lifuatalo:

Ingizo ni *ninakwenda [adhhabu]* (اذهب) na *[nda]* *Knf1uKwo

| **Ingizo** | **Maumbo Shindani** | ***Knf1uKwo** | **FIKI-UKO** | **TEGE** | **SHABI** |
|---|---|---|---|---|---|
| *adhhabu* na *nda* | *a) anadhhab, anada* | *! | | | * |
| | *b) anadhhb, anda* | *! | * | | * |
| | ☛*c) adhhab, nda* | | | | |
| | *d) adhhabu, nada* | | * | * | * |
| | *e) dhahab, nada* | | * | * | * |

Katika Jedwali hilo, maumbo (a) yamezingatia masharti mengi hafifu ya FIKI-UKO na TEGE lakini yamevunja sharti moja lenye nguvu la *Knf1uKwo hivyo, hayakuweza kufikia upeo wa ukubalifu. Mambo (b) yamevunja sharti lenye nguvu la kuruhusu kiambishi cha wakati uliopo baada ya kiambishi cha nafsi ya 1 umoja. Maumbo (c) hayakuvunja masharti hafifu ya FIKI-UKO, TEGE na SHABI wala sharti kubwa lenye nguvu hivyo, maumbo hayo ndiyo yanayokubalika kwa kuwa hayakuvunja masharti yoyote. Maumbo (d) na (e) hayakubaliki kwani yamevunja masharti hafifu ya FIKI-UKO, TEGE na SHABI.

Kitenzi kingine kilichoshughulikiwa katika ujitokezaji wa nafsi kwa wakati uliopo ni *tunakwenda.* Katika Kiswahili kiambishi *tu-* kinaonesha nafsi ya 1 wingi na kiambishi *na-* kinaonesha wakati uliopo. Wakati katika Kitumbatu *(tunda) tu-* kinaonesha nafsi ya 1 wingi na pia kinaonesha wakati uliopo kama ilivyo katika Kiarabu. Aidha, katika Kiarabu *nadhhabu* (نذهب) -نَ*(na)* kinaonesha nafsi ya 1 wingi pamoja na wakati uliopo. Shartizuizi hili linaweza kupangiliwa na UU kama ifuatavyo:

*Knf1wKwo >> FIKI-UKO >> TEGE >> SHABI

*KNf1wKNo Kiambishi nafsi ya kwanza wingi hakiwezi kufuatiwa na kiambishi cha njeo ya wakati uliopo

Data ifuatayo inatumika kama sampuli ya kutathmini maumboghafi katika Jedwali Na. 4:
Ingizo ni *tunakwenda [nadhhabu] (نذهب)* na *[tunda]* *Knf1wKwo

| **Ingizo** | **Maumbo Shindani** | ***Knf1wKwo** | **FIKI-UKO** | **TEGE** | **SHABI** |
|---|---|---|---|---|---|
| *nadhhabu,tunda* | *a) nanadhhab,tunanda* | *! | | * | |
| | *b) nadhhabi,tunandi* | | | * | * |
| | *c) nanadhab, tunand* | *! | * | * | * |
| | ☛*d) nadhhabu, tunda* | | | | |

Maumbo (a) na (c) yamevunja mashartizuizi yenye nguvu kwa kuingiza kiambishi cha wakati uliopo baada ya kiambishi cha nafsi ya kwanza wingi. Vilevile maumbo hayo yamevunja masharti ya FIKI-UKO, TEGE na SHABI yanayovumilika. Maumbo (b) yamezingatia sharti lenye nguvu la *Knf1wKWo hata hivyo, yamevunja masharti ya TEGE na SHABI. Maumbo (d) ndiyo yanayokubalika kwa utaratibu wa lahaja ya Kitumbatu na lugha ya Kiarabu kwa kuwa hayakuvunja sharti lenye nguvu pamoja na masharti yanayovumilika.

Kitenzi *anakwenda* katika Kitumbatu *kanda* kiambishi *ka-* kinaonesha nafsi ya 3 umoja pia njeo ya wakati uliopo. Kadhalika katika Kiarabu neno *tadhhabu* (تذهب) kiambishi cha nafsi ya 3 umoja *ta* - ت kina kazi mbili kwanza, kinawakilisha nafsi ya 3 umoja pili, njeo ya wakati uliopo. Hii ni tofauti na Kiswahili ambapo kiambishi *a-* kinawakilisha nafsi ya 3 umoja wakati *na-* kinawakilisha njeo ya wakati uliopo. Sharti hili tunaweza kulibainisha kama ifuatavyo:

*Knf3uKwo >> FIKI-UKO >> TEGE >> SHABI

*Knf3uKNjo kiambishi nafsi ya 3 umoja hakiwezi kufuatiwa na kiambishi cha njeo ya wakati uliopo

Tuchunguze data ifuatayo katika Jedwali Na. 5:

Ingizo ni *anakwenda [tadhhabu] tadhhabu (تذهب) na [kanda]* *Knf3uKwo

| **Ingizo** | **Maumbo Shindani** | ***Knf1wKwo** | **FIKI-UKO** | **TEGE** | **SHABI** |
|---|---|---|---|---|---|
| *tadhhabu na kanda* | ☛*a)tadhhabu, kanda* | | | | |
| | *b) nadhhabi, kandi* | | | * | * |
| | *c)tanadhab,akanda* | *! | * | | * |
| | *d)tadhihabu,kanida* | | * | | * |

Katika Jedwali Na. 6 mumbo (a) yamezingatia masharti hafifu ya FIKI-UKO, TEGE na SHABI pamoja sharti moja lenye nguvu la *KNf3uKwo hivyo, umbo hilo ndilo linalokubalika kwa kuwa halikuvunja masharti yoyote. Maumbo (b) na (d) yangeweza kukubalika kwa kuwa yamevunja masharti hafifu ya FIKI-UKO, TEGE na SHABI. Hata hivyo yameshindwa kwa kuwapo mumbo (a) ambayo hayakuvunja sharti lolote. Maumbo (c) hayakuweza kufikia upeo wa ukubalifu kwa kuwa yamevunja sharti lenye nguvu la *KNf3uKwo ambalo halikubaliki katika Kitumbatu na Kiarabu.

Ujitokezaji wa viambishi vya nafsi ya 1 umoja na wingi pamoja na kiambishi cha nafsi ya 3 umoja katika Kitumbatu na Kiarabu unatofautiana na Kiswahili. Hii ni kwa sababu viambishi vyake katika nafsi hizo, vinafanya kazi mbili kwa wakati mmoja. Pia viambishi hivyo katika Kiarabu vinawakilishwa na fonimu moja tu wakati katika Kitumbatu na Kiswahili, vinawakilishwa na silabi mbili tofauti.

**Kiambishi Nafsi cha Wakati Uliopita**

Kwa mujibu wa Masebo na Nyangwine (2002:199) wanaeleza kuwa vitenzi vya wakati uliopita katika Kiswahili, vinawakilishwa na *-li* na *ku.* Kiambishi *ku,* kinatumiwa pamoja na vitenzi vinavyokanushwa ambavyo huambatana na kiambishi kanushi *si-ha/hu*. Viambishi hivi vinajuilisha kuwa tendo lililotokea na kumalizika katika wakati uliopita. Ujitokezaji wa nafsi katika vitenzi vya wakati uliopita ni kama ufuatavyo katika mfano wa 5:

| Kiarabu | Kitumbatu | Fasiri ya Kiswahili |
|---|---|---|
| *dhahabtu (ذهبت)* | *nyende* | *nilikwenda* |
| *dhahabna (ذهبن)* | *twende/tulinda* | *tulikwenda* |
| *dhahaba (ذهب)* | *kwende* | *alikwenda* |
| *sharibta (شَرِبْتَ)* | *unywi* | *ulikunywa* |
| *kataba (كَتَبَ)* | *kandiki* | *aliandika* |

Tuangalie jinsi kiambishi cha nafsi ya 3 umoja kinavyojitokeza katika kitenzi *aliandika* (كَتَبَ) *kandiki* cha Kiarabu na Kitumbatu.

Katika Kiswahili kiambishi cha nafsi na kiambishi njeo vinajidhihirisha bayana katika wakati uliopita. Neno *aliandika* limejengeka kwa viambishi awali cha nafsi ya 3 umoja *-a-* na kiambishi njeo *-li-* cha wakati uliopita. Katika Kiarabu, neno hilo lina umbo moja tu, kiambishi cha nafsi ya 3 umoja *-a-* na kiambishi cha wakati *-li-* havionekani. Kitumbatu kiambishi *ka* kinafanya kazi ya nafsi ya 3 umoja na pia kinaonesha wakati uliopita. Tofauti hizi zinadhirisha wazi ya kwamba kila lugha ina masharti na vigezo vyake pekee vinavyotumika katika uundaji wa maumbo mbalimbali ya maneno kama ilivyoelezwa katika nadharia ya UU katika mhimili wa masharti zuizi.

*Knf3uHwp >> FIKI-UKO >> TEGE >> SHABI

*Knf3uHwp Kiambishi nafsi ya tatu umoja hakionekani katika cha wakati ulipita

Tuchunguze Jedwali Na. 6 lifuatalo:

Ingizo *aliandika [kataba]* (كَتَبَ) na *[kandiki]* *Knf3uHwp

| Ingizo | Maumbo Shindani | *Knf3uHwp | FIKI-UKO | TEGE | SHABI |
|---|---|---|---|---|---|
| *kataba na kandiki* | *a) akataba, akandiki* | *! | | * | * |
| | ☛*b)kataba, kandiki* | | | | |
| | *c) katabat, kandik* | | * | * | * |
| | *d) nakataba, na akandiki* | *! | * | * | * |

Katika kielelezo cha hapo juu, maumbo (a) yamevunja sharti lisilovumilika na lenye nguvu la *Knf3uHwp pamoja na masharti hafifu ya TEGE na SHABI hivyo maumbo hayo hayakubaliki. Maumbo (b) yamekuwa mshindi kwa kuwa yamezingatia masharti yote. Maumbo (c) yamevunja

masharti ya FIKI-UKO, TEGE na SHABI kadhalika hayakubaliki katika utaratibu wa lugha hizo. Maumbo (d) yamevunja sharti kubwa (*Knf3uHwp) pamoja na masharti ya FIKI-UKO, TEGE na SHABI; hivyo nayo hayakubaliki.

Kitenzi kingine ambacho kimeshughulikiwa katika kuonesha nafsi ya wakati uliopita ni *sharabta* (شَرِبْتَ) na u*nywi* (ulikunywa). Kitenzi *ulikunywa* katika Kitumbatu kiambishi *u-* kinaonesha nafsi ya 2 umoja kimeunganishwa na kiambishi cha wakati uliopita, yaani kiambishi cha wakati ulipita hakijidhihirishi bayana. Aidha, katika Kiarabu kiambishi cha nafsi ya 2 umoja -تَ kimenganishwa na mzizi شَرِبْ (*sharib)* na *-ta-* na kuwa neno lisilonyambulika. Vilevile, katika Kitumbatu neno *unywi* lina maumbo 3 *u-* kiambishi cha nafsi ya 2 umoja, *ny-* mzizi na *wi-* kiambishi tamati. Katika Kiswahili kiambishi cha nafsi ya 2 umoja *u-* na kiambishi cha wakati uliopita *li-* vinajidhihirisha bayana katika kitenzi hicho. Utofauti huu unathibitisha uhalisia wa nadharia ya Umbo Upeo katika mhimili wa mashartizuizi kuwa kila lugha huwa na vigezo na masharti yanayowaongoza watumiaji wa lugha husika katika uundaji wa maumbo sahihi ya maneno kwa kutumia viambishi mbalimbali.

*Knf2uKwp >> FIKI-UKO >> TEGE >> SHABI

*Knf3uKwp Kiambishi nafsi ya tatu umoja hakiwezi kutangulia kiambishi cha wakati ulipita

Tuchunguze jinsi maumbo shindani yanavyoonekana katika Jedwali Na. 7 lifuatalo;

Ingizo *ulikunywa [sharabta]* (شَرِبْتَ) na *[unywi]* *Knf2uKwp

| **Ingizo** | **Maumbo Shindani** | ***KNf2uMZwp** | **FIKI-UKO** | **TEGE** | **SHABI** |
|---|---|---|---|---|---|
| *sharibta na unywi* | *a)talisharibu, ulinwyi* | *! | | * | * |
| | ☛*b) sharibta, unywi* | | | | |
| | *c) shariba, unanywi* | | * | * | * |
| | *d) tashiribti, ulinanywi* | *! | * | * | * |

Maumbo (a) na (d) yamevunja mashartizuizi yenye nguvu kwa kuruhusu kiambishi cha nafsi ya 2 umoja kutanguliwa na kiambishi cha wakati uliopita. Vilevile maumbo hayo yamevunja masharti ya TEGE na SHABI yanayovumilika. Maumbo (c) yamezingatia sharti la *Knf2uKwp lakini yamevunja masharti ya TEGE na SHABI. Maumbo (b) ndiyo yanayokubalika kwa utaratibu wa lugha hizi kwa kuwa hayakuvunja sharti lolote.

**Kiambishi Nafsi cha Wakati Ujao**

Njeo ijayo ni njeo ambayo hueleza tendo ambalo litafanyika au kutofanyika katika wakati ujao Mgullu (1999). Mofu ambayo inatumika kuwakilisha njeo ijayo ni *-ta-*. Kiambishi *-ta-* kinatumika katika sentenzsi yakinishi na kanushi. Pia kiambishi hiki kinaonesha kuwa tendo litafanyika wakati ujao: Hebu tutalii ujitokezaji wa nafsi katika vitenzi vya wakati ujao kama unavyojidhihirisha katika mfano wa 6 ufuataao:

| **Kiarabu** | **Kitumbatu** | **Fasiri ya Kiswahili** |
|---|---|---|
| utakunywa (سَتَشْرَبُ) | utanywa | utakunywa |
| sayaakulu ( سَيَأْكُلُ) (me) | katalya | atakula |
| sayaktubu (س-يَ-كْتُبُ) | katandika | ataandiaka |
| sausafiri (سوسفـر) | tasafiri | nitasafiri |

Ujitokezaji wa viambishi cha nafsi katika wakati ujao unatofautiana baina ya Kitumbatu, Kiarabu, na Kiswahili. Katika Kiarabu, kiambishi cha nafsi ya 2 umoja -ت katika neno *satashrabu (سَتَشْرَبُ) (utakunywa)* kimejtikeza peke yake yaani kimetengana na kiambishi cha wakati ujao -سَ *(sa)* wakati katika Kitumbatu na Kiswahili kiambishi hicho ya nafsi ya pili umoja *u-* kimeungana na kiambishi cha wakati ujao *ta-*. Aidha, kiambishi cha wakati ujao katika Kiarabu -سَ kimejitokea mwanzoni kikiambatana na kiambishi cha nafsi cha 2 umoja -ت wakati katika Kitumbatu na Kiswahili kiambishi

cha wakati ujao *ta-* kimetanguliwa na kiambishi cha nafsi ya 2 umoja *u-*. Hii ni kwa mujibu wa Prince na Smolensky mwaka (1993) waasisi wa Nadharia ya UU kwamba ni lazima kuzingatia masharti na vigezo vinavyotakiwa kulingana na lugha husika.

*Knf3uKwj >> FIKI-UKO >> TEGE >> SHABI

*Knf3uKwj Kiambishi nafsi ya tatu umoja hakiwezi kutanguliwa na kiambishi cha wakati ujao katika Kiarabu.

Tuchunguze jinsi maumbo shindani yanavyoonekana katika Jedwali Na. 8:

Ingizo *utakunywa [satashrabu]* (سَتَشْرَبُ) na *[utanywa]*

| **Ingizo** | **Maumbo Shindani** | *Knf3uKwj | **FIKI-UKO** | **TEGE** | **SHABI** |
|---|---|---|---|---|---|
| *satashrabu na utanywa* | *a) tasashrabu* | *! | | | |
| | *b) satasharibu* | | | * | * |
| | ☛*c) satashrabu* | | | | |
| | *d) tasashribi* | *! | * | * | * |

Katika jedwali hilo, umbo (a) limezingatia masharti mengi hafifu ya FIKI-UKO, TEGE na SHABI lakini limevunja sharti moja lenye nguvu la *KNf3uKwj hivyo, halikuweza kufikia upeo wa ukubalifu. Umbo (b) limevunja masharti mawili hafifu ya TEGE na SHABI hata hivyo halikuweza kushinda kwa kuwa kuna umbo (c) ambalo halikuvunja masharti yoyote. Umbo (d) limevunja sharti lenye nguvu pamoja na masharti hafifu ya FIKI-UKO, TEGE na SHABI.

Kitenzi kingine kilichoshughulikiwa katika ujitokezaji wa nafsi kwa wakati ujao ni *sayaakulu (سَيَأْكُلُ)* na *katalya (atakula).*

Kama ambavyo tumeeleza hapo kabla kwamba, kuna tofauti ya mahali pa utokeaji wa kiambishi cha nafsi na kiambishi cha wakati ujao. Katika Kiarabu kiambishi cha wakati ujao kimejitokeza mwanzoni kabisa kama kiambishi awali -سَ *(sa)* kikifuatiwa na kiambishi cha nafsi ya tatu umoja -يَ *(ya)*; ilhali katika Kitumbatu na Kiswahili, kiambishi cha wakati ujao *ta-* kimejitokeza baada ya kiambishi cha nafsi ya tatu umoja *u-*. Hali hii ya utofauti wa maumbo na mahali pa utokeaji wa viambishi kinadhihirisha kile kilichosemwa na Prince na Smolensky mwaka (1993) waasisi wa Nadharia ya Umbo Upeo kwamba, ni lazima kuzingatia masharti na vigezo vinavyotakiwa kuzingatiwa wakati wa upachuikaji wa viambishi kulingana na lugha husika.

**Hitimisho**

Makala haya yamejadili kuhusu ujitokezaji wa viambishi vya nafsi katika Kiarabu, Kitumbatu na Kiswahili. Katika utafiti huu imebainika kuwa ujitokezaji wa viambishi vya nafsi katika Kiarabu unajitofautisha ukilinganishwa na Kitumbatu pamoja na Kiswahili kwa baadhi ya vitenzi. Mathalali viambishi vya nafsi ya kwanza umoja kwa wakati uliopo katika Kiarabu, unawakilishwa na kiambishi *-a-,* Kitumbatu kiambishi *-n-* na Kiswahili kiambishi *ni.* Vilevile, kiambishi cha nafsi ya 2 wingi katika Kiarabu kinawakilishwa na kiambishi *-a-* wakati katika Kitumbatu na Kiswahili huwakilishwa na kiambishi *tu.* Pia, tumeona kuwa kiambishi cha nafsi ya 2 umoja katika wakati uliopita, Kiarabu huwakilishwa na kiambishi *-sha-* ambapo katika Kitumbatu na Kiswahili huwakilishwa na kiambishi - *u-*

Katika utafiti huu vilevile imebainika kwamba, kuna utofauti wa mazingira ya utokeji wa viambishi vya nafsi katika Kiarabu. Kwa mfano kiambishi cha wakati ujao katika Kiarabu kinajitokea mwanzoni kikiambatana na kiambishi cha nafsi cha 2 umoja wakati katika Kitumbatu na Kiswahili kiambishi cha wakati ujao hutanguliwa na kiambishi cha nafsi ya 2 umoja. Kwa ujumla ujitokezaji wa viambishi vya nafsi katika Kiarabu unatofautiana kwa kiasi kikubwa na Kitumbatu pamoja na Kiswahili. Hii ni kudhihirisha kwamba Kiarabu na Kiswahili ni lugha mbili tofauti. Mathalani, kama tulivyotangulia kusema Kiarabu kina nafsi 12 katika umoja na wingi ambazo baadhi yake zinajitofautisha jinsi ya kike na kiume. Hali hii haijitokezi katika Kiswahili, kwa kuwa kina aina 3 tu za nafsi katika umoja na wingi. Hata hivyo, tunakubaliana na wataalamu wanaodai kuwa Kiswahili na

Kiarabu zimeathiriana kwa kiasi kikubwa katika kipengele cha msamiati. Hali ambayo imetokana na muingiliano pamoja na muwasala wa muda mrefu wa jamii mbili hizo, na sio kwamba Kiswahili kimetokana na Kiarabu. Kama ingekuwa hivyo lugha hizo zingekuwa na mwathiriano japo mdogo wa ujitokezaji wa viambishi katika vitenzi vyake mbalimbali. Hivyo, kwa kuwa lugha hizo hazitokani na lugha moja ya azali, kipengele hiki kimeonesha utofauti mkubwa baina ya Kiarabu na Kiswahili. Aidha, ujitokezaji wa viambishi vya nafsi katika Kitumbatu umeelekea kulingana kwa kiasi fulani na Kiswahili kuliko Kiarabu. Hii inatokana na ukweli kwamba Kitumbatu ni miongoni mwa lahaja za Kiswahili.

**Marejeleo**

Aghel, A. M. (2021). *Ulinganishi wa Mofolojia ya Vitenzi vya Kiswahili na Kiarabu*. Tasnifu ya Uzamivu [Haijachapishwa]. Chuo Kikuuu Huria cha Tanzania.

BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha.* Oxford University Press.

Chomi, E. W. (2013). *Kitangulizi cha Mofolojia ya Kiswahili.* TUKI.

Chomi, E. W. (2013). *Muundo wa Viambajengo vya Sentensi za Kiswahili.* TUKI. Z

Dawson, C. (2007). *A Practical Guide to Research Methods.* How to Book Limited.

Habwe, J. na Karanja, P. (2012). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Phoenix Publishers.

Juma, H. K. (2019). *Ulinganishi wa Kihistoria na Kiisimu wa Lahaja za Kiamu, Kimvita, Kipemba, Kitumbatu na Kimakunduchi. Tasnifu ya Uzamivu* [Haijachapishwa]. Chuo Kikuuu cha Dar es Salaam.

Khamis, A. B na Kiango, G. C. (2002). Uchanganzi wa Sarufi ya Kiswhili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kihore, Y. M. na wenzake (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo.* TUKI.

Masebo, J. A. & Nyangwine, N. (2006). *Nadharia ya Lugha: Kiswahili 1.* Nyambari Nyangwine Publishers

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha.* TUKI.

Massamba, D. P. B. (2017). *Historia ya Kiswahili. Mtazamo Mpya 100KK Hadi 2000BK.* Kiswahili Development Ltd.

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia; Kwa Sekondari, Vyuo Vikuu vya Kati na Vyuo Vikuu*. Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

McCarthy, J. & Prince A. (1993). Prosodic Morphology 1: Constrain Interaction and Satisfaction. In *Technical report No. 3* Amherst. University of Massachusetts and new Brunswick N. J Rutgers University.

McCarthy, J. & Prince, A. (1993). Prosodic Morphology 1: Constrain Interaction and Satisfaction. In *Technical report No. 3* Amherst. University of Massachusetts and New Brunswick N. J Rutgers University.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahii.* Longhon Publishers.

Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu.* Central Tanganyika Press.

Prince, A. & Smolensky, P. (1993). *Optimality Theory: Constraint Interaction in Generative Grammar*. Oxford.

Rubanza, Y. I. (1996). *Mofolojia ya Kiswahili.* Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Rubanza, Y. I. (2003). *Sarufi Mtazanmo wa Kimuundo.* Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.